

**WATUMISHI HOUSING COMPANY YASHAURIWA  
KUTENGA NYUMBA ZA KUWAUZIA NA  
KUPANGISHA WADAU WA MIFUKO YA HIFADHI YA  
JAMII**

Na Aaron Mrikaria- Dar es Salaam

21/03/2020

Menejimenti ya *Watumishi Housing Company* yashauriwa kutenga baadhi ya nyumba zilizojengwa na kampuni hiyo kwa ajili ya kuwapangisha Wadau wa Mifuko ya Jamii ili nao wanufaike na Mradi huo wa Nyumba za bei nafuu.

Ushauri huo umetolewa na Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ta Utumishi wa umma na Utawala Bora, Dkt. Mary Mwanjelwa (Mb) wakati wa ziara yake ya kikazi leo alipotembelea mradi wa nyumba wa kampuni hiyo katika eneo la Gezaule Wilaya ya Kigamboni mkoani Dar es Salaam.

**“Kutokana na uhalisia kwamba fedha za ujenzi wa Mradi wa Nyumba hizi unatokana pia na mchango wa fedha za wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, ni vema nao wakanufaika kwa kuuziwa baadhi ya nyumba hizi, kwa maana hiyo tutakuwa tumetenda haki kwa Watumishi wa Umma lakini pia tutakuwa tumetenda haki kwa wadau wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.”**

Aidha, Dkt. Mwanjelwa ameitaka Menejimenti ya *Watumishi Housing Company* kumchukulia hatua za

kisheria mkandarasi anayejenga tangi la maji katika mradi huo (CRJE) kutoka nchini China, endapo atashindwa kumaliza kazi hiyo kwa wakati.

Pia, Dkt. Mwanjelwa ameiagiza kampuni hiyo kuanza kumkata mkandarasi Hugo fedha za malipo ya kazi hiyo kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba kama njia mojawapo ya kutoa fundisho kwa wakandarasi wanaozembea kumaliza ujenzi wa miradi kwa wakati.

Sanjari na hayo, Dkt. Mwanjelwa ameipongeza *Watumishi Housing Company* kwa ubunifu wa kujenga nyumba za gharama nafuu, na kati ikiwa ni pamoja na kutoa fursa kwa wananchi kupanga katika nyumba hizo.